# YESMARK TUITION SERVICES

**102/2**
**KISWAHILI**
**KIDATO CHA NNE**
**KARATASI YA 2 - LUGHA**
**MWAKA WA 2016**
**MUDA: SAA 2 ½**

1. Maagizo.
   (a) Andika **jina lako** na **namba yako** ya usajili katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
   (b) Yajibu maswali yote. Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki..
   (c) Usitoe ukurasa wowote kutoka kenye kijitabu hiki.
   (d) **Karatasi hii ina kurasa 9 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za kratasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

www.yesmarkeducation.com

## 1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Mageuzi yanayotarajiwa katika idara ya polisi nchini yameanza kubisha hodi baada ya kuzinduliwa kwa mtaala mpya wa kutoa mafunzo kwa maafisa wa polisi.

Mtaala huo uliozinduliwa rasmi na Waziri wa Usalama wa Ndani Prof. George Saitoti Jumatatu iliyopita unalenga kuimarisha utenda kazi katika kikosi ambacho kwa muda mrefu kimelaumiwa kwa kukolewa ufisadi na uvunjaji haki za kimsingi.

Akihutubu katika hafla ya kuzindua mtaala huo, iliyofanyika katika makao makuu ya shirika la ndege nchini mtaani Embakasi, Nairobi, Waziri Saitoti alisema kuzinduliwa kwa mtaala huo kuliashiria mwanzo wa mageuzi makubwa yanayonuiwa kukipatia kikosi hico sura mpya.

"Nyakati zimebadilika na tutawapa maafisa wa polisi mafunzo mapya. Tunataka kuunda kikosi imara chenye nidhamu, kinachoheshimu haki za kibinadamu. Tunataka kuwa na kikosi kinachoakis isura ya karne hii na kinachofikia hadhi ya kimataifa." Alisema Waziri Saitoti.

Mtaala huo mpya wa kutoa mafunzo kwa maafisa wa polisi ni matunda ya jopo lililoteuliwa na Rais mwaka wa 2003, kutathmini mageuzi katika kikosi hicho. Uliandaliwa na Taasisi ya Elimu nchini ikishirikiana na wakufunzi kutoka Chuo cha Mafunzo ya Polisi cha Kiganjo kwa usaidizi wa wataalamu wa maswala ya usalama kutoka Uswizi.

Chini ya mtaala huo, maafisa wa polisi watapokea mafunzo kwa kipindi cha kati ya miezi 15-21. Kinyume na awali ilipowachukuwa miezi 9 tu kukamilisha mafunzo.

Aidha, alama za kujiunga na kikosi hicho zimeongezwa. Katika mtaala huo, wanaonuia kujiunga na idara ya Polisi wa Kawaida, kitengo cha GSU au Polisi wa Utawala, ni lazima wawe wamepata alama ya C katika mtihani wa KCSE na itachukuwa miezi 15 kukamilisha mafunzo ikiwa ni pamoja na miezi 3 ya kujifahamisha na huduma za kikosi.

Hii ni tofauti na awali ambapo alama ya kujiunga na kikosi cha polisi ilikuwa ni D katika KCSE. Mtaala mpya unasema ni sharti asilimia 10 ya makurutu wawe na digrii kutoka chuo kikuu na watapokea mafunzo kwa miezi 21 na kuhitimu cheo cha naibu inspekta wa polisi.

Na kuanzia sasa, sharti usawa wa kijinsia uzingatiwe kikamilifu katika uajiri wa maafisa wa polisi. Wachanganuzi wa masuala ya usalama wanasema ukizingatiwa ipasavyo, mtaala huo utasaidia kuunda msingi thabiti wa kikosi imara ambacho Wakenya wamekuwa wakihitaji.



www.yesmarkeducation.com

Maswali:

a) Ni dalili ipi inayoonyesha mwanzo wa mageuzi? (al. 1)

..........................................................................................................................................................................................

..........................

b) Mtaala mpya unalenga nini? (al. 4)

..........................................................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................................................

.....................................................

c) Eleza lawama zinazoelekezewa kikosi cha polisi. (al. 2)

..........................................................................................................................................................................................

...................................................................................................................................................

d) Kwa mujibu wa taarifa hii, eleza mambo matatu yanayokusudiwa kuletwa na mtaala mpya. (al. 3)

..........................................................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................................................

.....................................................

e) Taja makundi mawili yaliyohusika katika kuandaa mtaala mpya. (al. 2)

..........................................................................................................................................................................................

..........................

f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika kifungu. (al. 3)

(i) Kubisha hodi-..................................................... ...............................

(ii) Kukolewa-.......................................................................................

(iii) Kinachoakisi-...................................................................................

**2. UFUPISHO: (ALAMA 15)**

www.yesmarkeducation.com

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayoihusu.*

Aina fulani za kansa huwapata zaidi waanaume. Kansa ya tezi-kibofu, koremeo nay a mapafu ni baadhi ya hizo. Kansa ya tezi-kibofu huwalenga zaidi wazee wa umri wa miaka sitini na zaidi. Je, umewahi kujiuliza sababu ya akina babu kwenda haja ndogo mara kwa mara? Hii ni dalili mojawapo ya kansa. Zingine ni ugumu wa kupitisha mkojo, ugumu wa kuanza kutoa mkojo, damu kwenye mkojo, maumivu ya mgongo na kadhalika. Mwisho, tezi-bofu huzidi kwa ukubwa na kufungia mkojo kutoka.

Kansa zinazowapata zaidi wanawake ni ya nyumba ya uzazi, ya mlango wa uzazi na maziwa. Kansa ya maziwa inatisha mno. Wanawake wenye umri wa miaka thelathini na mitano na zaidi wamo hatarini kuliko wote. Dalili za awali ni uvimbe unaohisika kwa ndani na maziwa kutoa usaha. Kansa ya maziwa hunea upesi na kuvimbukiza viungo vilivyo karibu kama vile mapafu, ini na kadhalika.

Ugonjwa huu hautambuliki kwa urahisi kwani mwanzoni, hausababishi uchungu wowote. Inapendekezwa kwamba ukaguzi wa mara kwa mara unaweza kusaidia kugundua kansa kabla haijakomaa na kusambaa kote mwilini. Dalili ya awali hupatikana katika kiungo husika.

Madaktari wanapendekeza mambo kadhaa. Kwanza ni ukaguzi wa kibinafsi kwenye viungo vilivyo na uwezekano mkubwa wa kuambukizwa. Kisha jambo lolote lisilo la kawaida kama uvimbe, ugumu wa kumeza na kadhalika, liwasilishwe mara moja kwa daktari. Daktari atafanya uchunguzi wakena kuamua ni lipi linalomfaa mhusika. Kadhalika, ushauri zaidi ni kuhusu aina ya vyakula na mitindo ya kisasa ya maisha. Vyakula vilivyojaa protini zipatikanazo katika nyama na mayai ni miongoni mwa vyakula hatari. Mafuta kutokana na mimea hupendekezwa. Uvutaji sigara, unywaji wa pombe na baadhi ya vipodozi vya kisasa vyenye zebaki huweza kuzidisha uwezekano wa kupata kansa. Tukizingatia masharti haya, tutaziba ufa na kujiepusha na kujenga ukuta.

Saratani ni kama sikio la kufa halisikii dawa. Ikigunduliwa mapema, matibabu huanzishwa kwa kutumia dawa, tibakemikali au tiba miale ambayo huzichoma kwa miale chembechembe zilizoambukizwa.

Ikizidi, lisilo budi hutendwa. Huwa hakuna tena budi kiungo kuondolewa kwa upasuaji ili kuokoa sehemu zingine za mwili na maisha kwa jumla. Kwani wahenga hawakushauri kukata pua ili kuunga wajihi?

www.yesmarkeducation.com

Maswali:

a) Fupisha aya tatu za kwanza. (maneno 60-65) (alama 7; utiririko 2)

Matayarisho:

..............................................................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................................................

..................................................................................................

Jibu:

..............................................................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................................................

..................................................................................................

b) Kwa kutumia maneno 45-50, eleza njia mbazo zinaweza kutumiwa kujikinga na ugonjwa wa kansa. (alama 5; utiririko 1)

Matayarisho:

..............................................................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................................................

..........................................................................

Jibu:

..............................................................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................................................

......................................................................... ...............

**3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**



www.yesmarkeducation.com

a) Eleza mfanano uliopo baina ya sauti /f/ na /v/. (al. 2)

..................................................................................................................................................................................................

..........................

b) (i) Eleza maana ya silabi wazi. (al. 1)

..................................................................................................................................................................................................

...........................

(ii) Andika neno moja lenye muundo wa silabi wazi. (al. 1)

................................................................................................................

c) Tunga sentensi kwa kutumia kitenzi 'linda' katika kauli ya kutendeka. (al. 1)

..................................................................................................................................................................................................

..............................

d) Tofautisha baina ya kielezi cha namna halisi na cha namna hali. (al. 2)

..................................................................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................................................................

....................................................

e) Andika kwa udogo-umoja hali ya mazoea. (al. 2)

Wagobo hawa wamebeba mabibo yao kuelekea madukani.

..................................................................................................................................................................................................

..........................

f) Tunga sentensi iliyo na muundo ufuatao wa maneno. (al. 2)

U+ W+ t+ V+ T+ E

..................................................................................................................................................................................................

...........................

g) Kanusha. (al. 2)

Mwambie Makasi kuwa akichelewa atanikosa.

www.yesmarkeducation.com

.....................................................................................................................................................................................

...........................

h) Onyesha uamilifu wa mofimu katika fungutenzi ‘kilivilia’. (al. 3)

.....................................................................................................................................................................................

.....................................................................................................................................................................................

.....................................................................................................................................................................................

...............................................................................

i) Andika kinyume. (al. 2)

Mwendapole alizama alipokuwa akichimba kisima cha Rafiki.

.....................................................................................................................................................................................

..........................

j) Eleza tofauti inayojitokeza baina ya sentensi zifuatazo. (al. 2)

i. Watoto wote watasomeshwa.

ii. Watoto wowote watasomeshwa.

.....................................................................................................................................................................................

...............................................................................................................................................

k) Andika katika usemi halisi. (al. 2)

Waziri wa Kilimo alituahidi angehakikisha kwamba mashamba yetu yamelimwa kufikia mwisho wa mwaka.

.....................................................................................................................................................................................

...............................................................................................................................................

l) Tambua aina za vishazi katika sentensi ifuatayo. (al. 2)

Jambazi ambaye alipigwa kwa bunduki alipelekwa garini akiwa na jeraha.

.....................................................................................................................................................................................

...........................

m) Viakifishi vilivyopo mabanoni vimetumikaje katika sentensi zifuatazo? (al. 2)

i. Alimtusi ***tusi baya akakasirika. (vinyota)



www.yesmarkeducation.com

..........................................................................................................................................................

........................

ii. Wema hauozi (hisani haiozi) nakwambia sikia. (parandesi)

..........................................................................................................................................................

........................

n) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi. (al. 4)

Mtu aliyepotea alipatikana ingawa hakuwa na mavazi.

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................

o) Ukitumia mizizi ya vitenzi uliyopewa amrisha ulivyoagiwa mabanoni. (al. 2)

i. -safiri- (umoja) ........................................................................

ii. -nyw- (wingi) ........................................................................

p) Bainisha aina za nomino katika sentensi ifuatayo. (al. 2)

Kuimba kwa Ubaya kuliwaudhi wengi sana.

..........................................................................................................................................................

........................

q) Andika matumizi mawili ya neno 'vile'. (al. 2)

..........................................................................................................................................................

........................

r) Taja, kwa kutolea mfano, miundo miwili ya nomino za ngeli ya U-I. (al. 4)

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

.................................................

**4. ISIMUJAMII (ALAMA 10)**

www.yesmarkeducation.com

Ngoma hii inawababamba sana wasee. Imeshika mpaka hata watoi mtaani waielewa. Nangos mob zinaitumia kama 'skiza tune'. Skiza kwa sekunde tano.

a) Taja sajili inayorejelewa hapa. (al. 1)

..........................................................................................................................................................

..........................

b) Huku ukirejelea kifungu hiki, eleza sifa nne za sajili uliyotaja. (al. 4)

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..................................................................................

c) Eleza dhana ya ujozilugha huku ukitoa mfano mmoja. (al. 2)

..........................................................................................................................................................

..........................

d) Eleza istilahi zifuatazo kama zinavyotumiwa katika isimujamii. (al. 3)

i. Misimu-

..........................................................................................................................

........................................................................................................................

ii. Lafudhi-

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

iii. Pijini-

..........................................................................................................................

........................ ...................................................................................................

www.yesmarkeducation.com